

Maswali Tutakayouliza Ukituma Ombi la UNM Care au Out-of-County Care

Kila mtu anayetuma ombi la UNM Care au Out-of-County Care atapewa Mwakilishi wa Huduma za Kifedha wa kumsaidia kujaza ombi. Tafadhalii tupigie simu ili kupanga miadi na Mwakilishi wako. Unapopiga simu, tujulishe iwapo ungependa kukutana naye ana kwa ana au kuwasiliana naye kwa simu.

Ili kupanga miadi yako, tafadhalii piga simu kwa **505 272-2521 au 877 909-6661** (bila malipo) Jumatatu hadi Ijumaa kati ya saa mbili asubuhi (8:00 am) ana saa kumi na moja jioni (5:00 pm). Tuna Wawakilishi wanaozungumza Kihispania, Kivietinamu na Kinavajo. Ikiwa mmoja wao hapatikani kukusaidia, tutakuunganisha na mkalimani anayetoa huduma kwa njia ya simu au video.

Tunatoa huduma za ukalimani katika zaidi ya lugha 200, ikiwemo Lugha ya Ishara ya Marekani. Huduma za mkalimani ni za bila malipo. Tunatakiwa kisheria kutoa mkalimani kwa mtu ye yeyote anayemhitaji.

Taarifa hii itakusaidia kujiandaa kwa miadi yako na Mwakilishi wako wa Huduma za Kifedha. Inaorodhesha aina za maelezo na hati tutakazohitaji ili kukamilisha ombi lako la UNM Care au Out-of-County Care.

Tutauliza kukuhusu

Tutakuuliza maswali kukuhusu. Kwa mfano

Je, unaitwa nani?

Je, anwani yako ni ipi? Nambari ya simu? Anwani ya barua pepe?

Je, tarehe yako ya kuzaliwa ni ipi?

Je, una bima ya afya? Ikiwa unayo, ni ya aina gani?

Tutauliza kuhusu ukubwa wa kaya

Kwa wagonjwa wenye umri wa miaka 18 na zaidi, kaya inajumuisha mgonjwa, mume/mke wake iwapo anaye na kila mtu ambaye mgonjwa anatarajia kudai kuwa mtegemezi katika maelezo ya kodi. Katika mipango hii miwili, mtu anayedaiwa kuwa mtegemezi katika maelezo ya kodi lazima awe anaishi nawe ili kuhesabiwa kama sehemu ya kaya yako.

Kwa wagonjwa wenye umri wa chini ya miaka 18, kaya inajumuisha mgonjwa, wazazi au walezi wake na kila mtu ambaye wazazi au walezi wake wanatarajia kudai kuwa ni mtegemezi katika maelezo ya kodi.

Ikiwa una maswali kuhusu wategemezi, tafadhali muulize Mwakilishi wa Huduma za Kifedha wakati wa mahojiano yako.

Tunaweza kuuliza maswali kama haya kuhusu watu wa kaya yako

Je, ni wanafamilia gani wanaishi katika kaya yako?

Je, kila mtu ana umri gani?

Je, kila mtu ana uhusiano gani na mgonjwa?

Je, kila mtu ana aina ipi ya bima ya afya (ikiwa ipo)?

Wewe ni Nani (Utambulisho)

Tutakuomba ulete 1 kati ya hati hizi kwa **kila mtu katika kaya yako**. Hati hizi hutusaidia kuthibitisha utambulisho wako na utambulisho wa kila mtu anayeishi nawe. Tutakubali yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapa chini (nakala pekee tafadhali).

Pasipoti (ya kigeni au ya Marekani)

Cheti cha kuzaliwa (cha kigeni au cha Marekani)

Kitambulisho cha picha (leseni ya dereva, kitambulisho kilichotolewa na serikali, kitambulisho cha kazi au cha shule)

Kadi ya mpango wa Social Security

Cheti cha Mzaliwa wa Kihindi

Hati za talaka

Fomu za malipo ya kodi ya mapato

Hati ya malipo ya Social Security, malipo ya ulemavu, malipo ya
uzeeni au malipo ya kustaafu

Taarifa kutoka kwa mhudumu wa kesi, mhudumu wa afya ya
jamii, mto huduma wa afya au shirika la jamii linalokujua na
linalojua hali yako

Ikiwa huna yoyote kati ya hati zilizoorodheshwa hapa, tunaweza

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili